NOT FOR SALE



## UBORESHAJI WA MAKAO DUNI

Serikali kutumia Sh1.2 bilioni kuboresha mitaa saba ya mabanda Kilifi UKURASA WA 8




## UMILIKI WA ARDHI

Wakazi zaidi ya 2,000 Rongai kupata hati miliki title baada ya kusubiri kwa miaka 31

UKURASA WA 23

## UHIFADI

Kaunti ya Kajiado sasa yatwaa usimamizi wa Mbuga ya Kitaifa ya Amboseli



UKURASA WA 25

www.mygov.go.ke

Novemba 19, 2024

YOUR WEEKLY REVIEW

MyGov.

Issue No. 21/2024-2025

# Serikali kujenga maabara katika shule za upili 2025

Katibu Mkuu wa Elimu ya Msingi, Dkt Belio Kipsang anaonngeza kwamba, serikali itajenga maabara 2,000 za mtandaoni kusaidia STEM wanafunzi wafunzi wa JSS wakjiunga na Darasa la Grade 10

NA **WANGARI MWANGI**, KNA

Serikali imetangaza mipango ya kujenga maabara 2,600 katika shule za sekondari kuanzia Januari 2025 kama sehemu ya maandalizi ya wanafunzi wa kwanza wa Shule za Upili chini ya Mtaala wa (CBC).

KKulingana na Katibu Mkuu wa Idara ya Serikali ya Elimu ya Msingi, Dkt. Belio Kipsang, maabara 1,600 zitajengwa katika shule za upili ambazo kwa sasa hazina vifaa hivyo. Serikali pia inapanga kuanzisha maabara 2,000 za kimtandao ili kusaidia elimu ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) wanafunzi watakapojiunga na Darasa la 10 baadaye 2026.

"Tumejitolea kuhakikisha kwamba kundi la kwanza la wanafunzi wa Darasa la 8 litakapoingia Darasa la 10, kila shule itakuwa na angalau maabara moja. Kuanzia Januari mwaka ujao, tutajenga maabara 1,600 katika shule za upili zilizopo, ambazo wanafunzi wataingia 2026," akasema Dkt. Kipsang.

"Tutaanzisha pia maabara 2,000 za mtandaoni, kuwezesha wanafunzi kushiriki masomo kwa vitendo katika maabara halisi huku pia wakinufaika na tekinolojia kupitia maabara za mtandaoni."

Juhudi hizi ni sehemu ya juhudi pana za serikali za kuanzisha mifumo inayohitajika ili kuimarisha na kutekeleza kikamilifu mtaala wa CBC.

ENDELEA UKURASA WA 2



Dkt Belio Kipsang

## AirAsia X sasa yatua Kenya




**Kenya yapiga hatua kubwa katika kuimarisha usafiri kati yake nceneo la Asia-Pasifiki baada ya kuwasili kwa ndege ya kwanza ya AirAsia X kutoka Kuala Lumpur, hadi Nairobi. Ndege hiyo ya kwanza ilibeba abiria 377, wakiwemo watalii, wafanyabiashara na wanafunzi, na ilikaribishwa kwa shangwe na maafisa wakuu wa serikali na sekta hiyo. Picha: Kwa Hisani**

## Wakenya 3,247 zaidi wapata kazi Qatar katika awamu ya pili

BY **CHRIS MAHANDARA,** KNA

Waziri wa Leba Alfred Mutua ametangaza shughuli ya kitaifa ya kusajili Wakenya wanaotaka kufanya kazi nje ya nchi.

Shughuli hiyo, itakayoanza Jumatano (kesho) katika Kaunti ya Machakos, inalenga kaunti zote 47 kufuatia nyingine ya hivi majuzi ambapo Wakenya 3,247 waliajiriwa na kampuni moja ya Qatar.

Dkt Mutua alisema uamuzi wa kuendesha shughuli hiyo katika kila kaunti umetokana na changamoto zilizokabili Wakenya wengi katika kusafiri hadi jumba la KICC na Chuo cha Kitaifa cha Ufundi cha Kabete.

"Tuligundua watu walitoka kila pembe ya nchi. Si haki kusafiri mbali huku baadhi yao wakilala katika vituo vya usajili. Badala yake tutawapelekea kazi hizo katika kaunti zote 47," akasema.



**Labour Cabinet Secretary (CS) Alfred Mutua addressing the media in Kisumu.**

Kampuni ya Qatar, ambayo awali ilitaka kuajiri watu 8,000, imerudi kuajiri Wakenya wengine 5,000 kwa nafasi zilizosalia. Dkt Mutua amewataka Wakenya watumie fursa hiyo na kujitokeza kufika kwa maeneo ya usajili katika

ENDELEA UKURASA WA 2

## Takwimu za Wiki

**8000**
Jumla ya idadi ya Wakenya ambao Kampuni ya Qatar inataka kuajiri katika maeneo mbalimbali kote nchini.

**900,000**
Idadi ya wakazi serikali ya kaunti ya Kericho inalenga kusajili na SHA

**60**
Megawati zaidi ambazo kampuni ya Kenya Electricity Generating Company (KenGen) imeweka katika mfumo wa kitaifa baada ya kufufua Kiwanda cha Gesi cha Muhoroni

**2,000**
Wakaazi watakaopokea hatimiliki kutoka kwa Wizara ya Ardhi kwa ushirikiano na Serikali ya Kaunti ya Nakuru baada ya kusubiri kwa miaka 31.

**1.2b**
Kiasi cha pesa ambacho Serikali itatumia kuboresha mitaa saba ya mabanda Kilifi chini ya KISIP 2

**2b**
Kiasi cha pesa ambacho serikali imetenga kusambaza wa tani 97,000 za mbolea ya ruzuku kwa wakulima wa chai.

# Kaunti 47 zalengwa katika usajili wa watu kwa ajira ughaibuni

ENDELEA KUTOKA UK 1

makao makuu ya kaunti kote nchini.

Aliongeza kuwa matifa mengine pia yameahidi kazi yakiwemo Ujerumani, Saudi Arabia, Australia, Austria, Jamhuri ya Czech, na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Maelezo kuhusu kazi hizo yatawekwa kwenye tovuti ya Wizara na tovuti nyingine za serikali.

Alisema nafasi hizo za kazi zitatolewa kwa mpango kuhakikisha kila kaunti imepata mgao wake wa haki.

Usajili katika kaunti utaendeshwa katika vyuo vya Mafunzo ya Ufundi (TVET) katika makao makuu ya kaunti. Hiyo itawezesha wanaotafuta kazi kufanyiwa majaribio ya ujuzi wao kulingana na kazi wanazotaka.

Dkt Mutua alisema maafisa wa Wizara wanaoongoza shughuli hiyo wataandamana na mashirika ya kuajiri yaliyosajiliwa na maafisa kutoka mashirika mengine husika ya serikali, wakiwemo wa Huduma ya Kitaifa ya Polisi (NPS) na Idara ya Uhamiaji. Ushirikiano huo unalenga kuharakisha utoaji wa vyeti vya maadili mema na pasipoti kwa watakaofaulu.

Shughuli hiyo katika kila kaunti, ambayo inalenga kuwapa kazi Wakenya wasiopungua milioni moja itaendeshwa kwa njia huru na wazi, na kutoa fursa sawa kwa Wakenya wote waliohitimu na wenye ujuzi.

Akihutubia wanahabari mjini Kisumu baada ya kuhudhuria kikao cha Kamati ya Idara ya Bunge kuhusu Leba, Dkt Mutua alisema kuwa aliwataka Wakenya wanaotafuta kazi nje ya nchi wajiandae kwa kuhakikisha stakabadhi zao ziko sawa.

"Wakati wa shughuli ya usajili hivi majuzi, wengine walikosa nafasi kwa sababu hati zao hazikuwa sawa. Wengine, kwa sababu ya uchovu na njaa, hawakuweza kufanya vizuri," akasema.

# Serikali kujenga maabara 2,600 katika shule zote za sekondari mwaka wa 2025

ENDELEA KUTOKA UK1



Akitoa taarifa ya hali ya utekelezaji wa Mfumo wa Elimu ya Msingi, Dkt. Kipsang alisema Wizara ya Elimu imeyarisha miongozo kuhusu jinsi wanafunzi wakavyojiunga na Darasa la 10.

Baada ya kumaliza mtihani wa Darasa la 9 mwaka ujao, wanafunzi watasajiliwa katika kimojawapo cha vitengo vitatu ya kuendeleza masomo: STEM (kwa watakaofanya vyema katika Hisibati na Sayansi), Sayansi ya Jamii, au Sanaa na Michezo.

Dkt. Kipsang alisema serikali inalenga kuwapa wanafunzi wote fursa ya kuendelea na masomo ya STEM wanajiunga na vyuo vinavyozingatia ujuzi. "Usajili hautakuwa wa moja kwa moja kama hapo awali, ambapo alama pekee ziliamua shule anayojiunga nayo mwanafunzi. Wakati huu itakuwa zaidi ya alama na kuumuisha kitengo ambacho mwanafunzi amechagua," akaelezea.

Wizara pia imetayarisha miongozo ya usimamizi wa Shule za Sekondari, ikiwatambua walimu wakuu wa shule za sekondari kama wadau muhimu katika kutekeleza mtaala wa CBC.

"Tunajiandaa kwa mpito wa mwisho kutoka Darasa la 9 hadi la 10. Huu ni wakati mwafaka wa kujadili jinsi ya kusimamia mpito huu kikamilifu. Punde tu mitihani ya Kidato cha Nne (KCSE) ikimalizika, tutashirikisha wakuu wa shule kukagua na kuboresha miongozo hio," akasema Dkt. Kipsang.

Katika kukabiliana na uhaba wa walimu, Dkt Kipsang alisema wizara inaimarisha uwezo wa walimu na inashirikiana na Tume ya Kuajiri Walimu (TSC) kuajiri walimu wa ziada kwa Shule za Sekondari za Chini (JSS).

Wizara inalenga kuwa na zaidi ya walimu 90,000 katika mfumo wa JSS ifikapo Januari 2025, huku tukilenga kuajiri walimu 120,000.

"Tunafanya kazi kwa karibu na TSC kuajiri walimu zaidi na kutathmini walimu waliopo wa shule za msingi ambao wanaweza kupandishwa hadhi kufundisha katika kiwango cha JSS.

Katika mwaka mmoja ujao, tunalenga kuwa na walimu wote walio na ujuzi unaohitajika," akasema.

Katibu Mkuu alikuwa akizungumza katika Shule ya Msingi ya Giakanja, Kaunti ya Nyeri, baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba vya Darasa la 9.


HIGHER EDUCATION LOANS BOARD
INVITATION TO TENDER
NATIONAL OPEN TENDER

The Higher Education Loans Board is a state corporation whose mandate is to source for funds and provide loans, scholarships and bursaries to Kenyans studying in recognized institutions of higher learning.

HELB invites interested, eligible Human Resource Recruitment Consultancy firms with relevant experience for the submission of sealed Request for Proposal as follows:-

| Tender Number | Tender Description | Tender closing date | Eligibility |
|---|---|---|---|
| HELB/RFP/05/2024-2025 | Provision of Human Resource Recruitment Consultancy | Wednesday 27th November 2024 11.00am | Open |

Interested and eligible firms may obtain further information and inspect the tender document at the Procurement office on 18th floor of Anniversary Towers, University Way, Nairobi during normal working hours or view and download the respective **detailed tender advert** and **tender document** from our website www.helb.co.ke/procurement/ or https://tenders.go.ke. All bidders interested in participating in the tender must notify HELB of their participation in the tender by emailing their contact details to procurement@helb.co.ke in case of any further tender addendum.

CHIEF EXECUTIVE OFFICER
HIGHER EDUCATION LOANS BOARD

EMPOWERING DREAMS

www.helb.co.ke Anniversary Towers University Way USSD *642#
+254711052000 contactcentre@helb.co.ke @HELBPAGE



REPUBLIC OF KENYA

THE NATIONAL TREASURY & ECONOMIC PLANNING

PUBLIC NOTICE

DRAFT PUBLIC FINANCE MANAGEMENT (DISASTER RISK MANAGEMENT FUND) REGULATIONS, 2024

The National Treasury and Economic Planning has been leading the process of developing the Public Finance Management (Disaster Risk Management Fund) Regulations, 2024 and these have been availed at the National Treasury website (**www.treasury.go.ke**).

Pursuant to Sections 4(a) and 5(3) (a) and (b) of the Statutory Instruments Act, 2013, the National Treasury and Economic Planning invites interested members of the general public to attend public consultations on the draft Regulations as per the schedule set out below: (Time for all sessions is from 9:00 a.m. to 1:00 p.m.)

| COUNTIES | VENUE | DATE |
|---|---|---|
| **CLUSTER A** | | |
| Mombasa City, Kwale, Kilifi, Tana River, Lamu and Taita Taveta | Mombasa City | Monday, 2nd December, 2024 |
| Isiolo, Wajir, Mandera, Marsabit, Garissa and Meru | Isiolo | Thursday, 5th December, 2024 |
| Nyeri, Embu, Kitui, Tharaka Nithi, Makueni and Kirinyaga | Nyeri | Monday, 9th December, 2024 |
| Nairobi City, Kiambu, Machakos, Murang'a and Kajiado | Nairobi City | Wednesday, 11th December 2024 |
| **CLUSTER B** | | |
| Kisii, Migori, Homabay, Nyamira, Kericho and Bomet | Kisii | Monday, 2nd December, 2024 |
| Kisumu City, Vihiga, Bungoma, Busia, Siaya and Kakamega | Kisumu City | Thursday, 5th December 2024 |
| Uasin Gishu, West Pokot, Trans Nzoia, Nandi, Baringo, Elgeyo Marakwet and Turkana | Uasin Gishu | Monday, 9th December, 2024 |
| Nakuru City, Laikipia, Narok, Nyandarua and Samburu | Nakuru City | Wednesday, 11th December, 2024 |

HON. CPA JOHN MBADI NG'ONGO, EGH
CABINET SECRETARY

KENYA VISION 2030

# Serikali yatenga Sh2b kwa mbolea ya ruzuku kwa wakulima wa chai

NA **FATMA SAID,** KNA

Serikali imetenga Sh2 bilioni kusambaza tani 97,000 za mbolea ya ruzuku kwa wakulima wa chai. Hatua hiyo inanuiwa kuzidisha mapato yao, kuwapunguzia gharama kwa wakulima na pia kuhakikisha wanapata pembejeo muhimu zinazohitajika ili kuboresha mavuno na ubora wa chai.

Akizungumza katika mkahawa wa Sarova Whitesands wakati wa mkutano wa kuadhimisha miaka 100 ya uuzaji wa chai wa Bodi ya Chai ya Kenya, Naibu Rais Kithure Kindiki, alisema kwamba, katika miaka miwili iliyopita, serikali imesambaza tani 180,000 za mbolea ya ruzuku kwa wakulima kwa Sh2,500 kwa kila mfuko wa kilo 50.

Kuhusu changamoto nyingine katika sekta hiyo, Naibu Rais alisema serikali imepiga hatua kubwa katika kutatua masuala ya uongozi katika Shirika la Ustawi wa Chai Kenya (KTDA) kupitia uchaguzi wa hivo majuzi ambao ulileta uongozi mpya.

Aliongeza kwamba mageuzi ya kisheria na kitaasisi yanaendelea ili kuimarisha utendakazi wa sekta hiyo na kwamba hatua zifaazo zitachukuliwa ili kulinda maslahi ya wakulima.

Kindiki aliongeza kwamba marekebisho ya Sheria ya Chai ya mwaka wa 2020 yanaendelea, huku baadhi ya kanuni za chai zinazotakiwa kutekeleza sheria hiyo zikiendelea kutayarishwa.

"Ili kulinda hadhi na sifa ya Chai ya Kenya na sekta hiyo na kuhakikisha uendelevu, serikali imeendelea kushughulikia changamoto zinazokabili uzalishaji chai, muhimu zaidi zikiwa gharama kubwa ya uzalishaji na utayarishaji, masoko, ukosefu wa thamani. kwa kuongeza, ubora wa chai na changamoto za kila mara kuhusu uongozi," akasema Kindiki.

Alisema kipaumbele cha serikali ya Kenya Kwanza kuhusu kilimo ni kurahisisha uzalishaji badala ya utumiaji. Aliongeza kwamba mpango huo mpana unalenga kuimarisha mapato ya kilimo, kuhakikisha usalama wa chakula, kutoa nafasi za ajira na kuongeza kuongeza mauzo ya nje ya Kenya.

Naibu Rais alisema chai ya Kenya inaaminika kuwa bora zaidi kote duniani kote kutokana na ubora wake, ladha nzuri na inaleta karibu Sh200 bilioni mapato ya kigeni kila mwaka, ambayo inachangia asilimia mbili ya Pato la Taifa (GDP). Inashikilia nafasi ya tatu baada ya mapato kutokana na Wakenya walio ugenini na Utalii.

"Chai ya Kenya ni nguzo kuu ya uendelevu na uhifadhi wa mazingira wa nchi yetu. Pia imesaidia sekta ya elimu na uchumi wa vijijini kama chanzo kikuu cha mapato na ajira," akasema Kindiki. Alitambua nafasi ya wanawake katika Sekta ya Chai, akisema wanachangia zaidi ya asilimia 60 ya uzalishaji wa chai duniani, na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uendelevu, tija, na maendeleo ya jamii, hasa kwa sababu uzalishaji chai unahitaji kazi nyingi.




**Naibu Rais Kithure Kindiki akihutibia alipoanzisha rasmi sherehe za kuadhimisha miaka 100 ya Bodi ya Chai ya Kenya (TBK) jijini Mombasa.**

"Ukuzaji cha pia unasaidia kilimo endelevu na uhifadhi wa mazingira, hivyo kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa sababu mojawapo ya hatari zinazokabili Sekta yetu ya Chai ni mabadiliko ya tabianchi, kuvurugwa kwa misimu na kuwepo kwa hali mbaya ya anga inayoathiri ubora wa chai," akasema.

Naibu Rais alisema kilo 600 milioni za chai huzalishwa Kenya kila mwaka huku akiahidi kuzidisha kiwango hicho kupitia sera zifaazo, ikiwepo utoaji wa mbolea ya kuhakikisha wadau wote, hasa wakulima wanafaidi kutokana na bidii yao.

Waziri wa Kilimo, Andrew Karanja, alisema serikali, kupitia Mpango wa Kubadilisha Uchumi wa Bottom-Up imeweka mbele kilimo cha Chai.

Alisisitiza umuhimu wa kuendelea kutatua changamoto muhimu zinazoikabili sekta ya chai, ili kuhakikisha uendelevu na ushindani wake. Miongoni mwa hayo ni umuhimu wa kuongeza thamani kwa bidhaa za chai, ili kuvutia soko la kimataifa na kuleta faida kubwa kwa wakulima.

---

**ampath** *Leading With Care*

*Academic Model Providing Access To Healthcare*
*Telephone: 254 53 2033471/2P.O. BOX 4606, ELDORET Fax: 254 53 2060727*

## TENDER NOTICE

AMPATH, a program under the auspices of Moi Teaching and Referral Hospital (MTRH), and Moi University invites sealed bids for the under- listed tenders.

**NATIONAL TENDERS**

| No. | Tender No. | Tender Description | Eligibility | Closing Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MTRH/AMP/T/28/2024-2025 | TENDER FOR RENEWAL OF ANNUAL LICENSES, SUPPORT AND MAINTENANCE OF ENTERPRISES SUITE – SOPHOS AND CYBERSECURITY MANAGED DETECTION AND RESPONSE(MDR) SOLUTION | RESTRICTED | 25th November 2024 |
| 2 | MTRH/AMP/T/29/2024-2025 | TENDER FOR THE MAINTENANCE OF AMPATH CCTV INFRASTRUCTURE | OPEN | 25th November 2024 |
| 3 | MTRH/AMP/T/30/2024-2025 | TENDER FOR THE PROVISION OF AMPATH ICT INFRASTRUCTURE PREVENTATIVE MAINTENANCE AND SUPPORT (HPE SERVERS, ACS, FIRE SUPPRESSION AND UPS) | OPEN | 25th November 2024 |

Complete sets of Tender documents shall be obtained by interested Bidders free of charge from MTRH official website: **www.mtrh.go.ke** and state tender portal: **www.tenders.go.ke**.

Tender bids in plain sealed envelopes bearing the Tender number (**in bold**) on the top right-hand corner but with no indication of the Tenderer's name should be deposited in **Tender Box "A"**, located at **Ground Floor, Chandaria Cancer Centre** or Posted to

**The Chief Executive Officer**
**Moi Teaching and Referral Hospital**
**P.O. Box 3-30100 ELDORET**

So as to be received on or before **25th November 2024 respectively, at 10.30 am.** Bids will be opened publicly immediately thereafter in the presence of Bidders or their representatives who choose to attend at **AMPATH Centre 1st Floor ATI Hall RM 118.** Late bids will not be accepted whatsoever and shall be returned unopened. Companies owned by Youth, Women and Persons with Disabilities are encouraged to participate.

All queries regarding this tender should be directed to the Supply Chain Manager - USAID AMPATH Uzima at **procurement-info@usaidampathuzima.or.ke** and copied to **acherotich@usaidampathuzima.or.ke**

**DR. PHILIP K. KIRWA,**
**CHIEF EXECUTIVE OFFICER**

KENYA VISION 2030

---

REPUBLIC OF KENYA

## MINISTRY OF TOURISM AND WILDLIFE

## STATE DEPARTMENT FOR WILDLIFE

### INVITATION TO TENDER

### TENDER FOR PROVISION OF COMPREHENSIVE CLEANING SERVICES

**TENDER NUMBER: MOTW/SDW/ONT/001/ 2024-2025**

The State Department for Wildlife invites sealed tenders for the Provision of Comprehensive Cleaning Services at NSSF Building Block 'A' 15th ,20th and 21st Floors.

Tendering will be conducted under open competitive method (National) using a standardized tender document. Tendering is open to all qualified and interested tenderers.

Tender documents containing detailed specifications can be downloaded free of charge from our website **www.tourism.go.ke** or **www.tenders.go.ke** and register for notifications for the tender in the **www.tenders.go.ke.**

Tenders shall be quoted in Kenya Shillings and shall include all taxes. Tenders shall remain valid for (**180**) days from the date of opening of tenders.

The Tenderer shall chronologically serialize all pages of the tender documents submitted.

Completed tenders must be delivered to the address below on or before **4th December, 2024. The Principal Secretary, State Department for Wildlife, P. O. Box 41394 - 00100,** and be deposited into the tender box at the State Department for Wildlife, NSSF Building, Block-A, Eastern Wing, 15th Floor, on or before **11:00 A.M, 4th December, 2024.**

Electronic Tenders will not be permitted.

Tenders will be opened immediately after the deadline date and time specified above or any deadline date and time specified later. Tenders will be publicly opened in the presence of the Tenderers' designated representatives who choose to attend at the address below.

Late tenders will be rejected.

**The addresses referred to above are:**
**The Principal Secretary,**
**State Department for Wildlife,**
**NSSF Building, Block-A, Eastern Wing, 15th Floor**
**P. O. Box 41394 - 00100, NAIROBI.**

**PRINCIPAL SECRETARY**

KENYA VISION 2030

# Chuo Kikuu cha Taveta chaungana na washikadau kuimarisha ujuzi wa wachimbaji madini wadogo

NA **GEORGE KAIGA**, KNA

Chuo Kikuu cha Taita Taveta (TTU) kimeanzisha mpango wa kuzidisha uwezo wachimbaji madini wadogo kote nchini.

Makamu wa Naibu Chansela anayesimamia Taaluma, Utafiti na Ushirikiano, Profesa Christine Onyango, alisema chuo hicho kimejikita katika kujenga uwezo wachimbaji madini wadogo ili kuboresha ujuzi wao wa kiufundi na usimamizi wa fedha ili kuongeza mapato yao.

Akizungumza katika hafla ya kwanza ya mpango huo mjini Kakamega, Profesa Onyango alisema eneo la Magharibi lina utajiri wa dhahabu, lakini mara nyingi wachimba madini wengi hunyonywa na wafanyabiashara wa kati ambao hununua madini yao ya thamani kwa bei duni.

Alifafanua kwamba, katika kukabiliana na changamoto hiyo, chuo hicho kikuu - kinachojivunia utaalamu katika uchimbaji madini na uhandisi wa utayarishaji - kimeshirikiana na wadau wengine kutoa mafunzo kwa wachimbaji madini wadogo katika masuala ya usimamizi na fedha, ili kuwawezesha kupata mapato bora kutokana na kazi yao kwa kuongeza thamani.

"Mara nyingi wachimbaji madini wadogo huuza dhahabu yao ya thamani kwa wafanyabiashara wa kati kutokana na ukosefu wa maarifa na hawapati thamani ya mapato yao," akasema Profesa Onyango.

"Wachimbaji wengi hawana ujuzi katika usimamizi, hawana ujuzi wa kutosha na wanatumia vifaa duni kuchima madini na kuhatarisha maisha yao," akasema.

Profesa Onyango alisema warsha hiyo pia iliangazia masuala ya usalama ikizingatiwa kwamba uchimbaji wa dhahabu nchini unahatarisha maisha kutokana na matumizi ya zebaki.

Zebaki hutumiwa kutenganisha dhahabu vitu vingine vingine lakini huleta hatari kubwa kwani inaweza kuharibu figo na uwezo wa kuona.

Alisema pia kuna athari mbaya za mazingira kutokana na uchimbaji madini ukiwemo ukataji miti na mabadiliko ya tabia nchi.

Profesa Onyango alisema chuo hicho kinalenga kusaidia jamii kukabiliana na athari mbaya za mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa yanayotokana na uchimbaji wa madini.

Akizungumza katika hafla hiyo, Maurice Juma Ogada, Profesa wa Uchumi wa Kilimo na Rasilimali Uchumi wa chuo hicho alisema taasisi hiyo inashirikiana na wafadhili na wadau wengine ili kuwapa wachimbaji madini wadogo ujuzi wa kutosha kuhusu usalama na uongezaji thamani.

Kupitia ufadhili kutoka kwa taasisi ya German Academic Service na kupitia Kituo cha Ubora cha Uhandisi wa Mazingira na Usimamizi wa Rasilimali (CEMERM), chuo hicho kikuu chenye makao yake makuu mjini Pwani kimeshirikiana na vyuo vikuu viwili vya Ujerumani - Chuo Kikuu cha Ufundi cha Madini mjini Freiberg na Chuo Kikuu cha Sayansi mjini Dresden kuboresha ujuzi na maarifa ya wachimbaji madini.

Profesa Ogada alisema TTU kitapeleka mpango huo katika maeneo mengine nchini ili kutoa ujuzi kwa wachimbaji madini wadogo kufuatia kuongezeka kwa visa vya ajali.

"Tunataka kuwafahamisha wachimbaji madini wadogo kuhusu athari ya kazi yao kwa mazingira na jinsi tunavyoweza kupunguza hatari na kukarabati maeneo ambayo uchimbaji madini umekuwa ukifanywa," akaongeza.



**Wachimbaji madini wadogo wakiingia katika mgodi kuchimba dhahabu katika eneo la Rosterman, Kakamega. Chuo Kikuu cha Taita Taveta kimeanzisha mpango wa ushirikiano unaolenga kutoa mafunzo kwa wachimbaji madini wadogo sehemu zote nchini. Picha na Moses Wekesa, KNA.**



**Makamu Naibu Chansela anayesimamia Masomo, Utafiti na Ushirikiano Profesa Christine Onyango akizungumza na Kenya News Agency mjini Kakamega. Picha na Moses Wekesa**

Warsha hiyo ya siku tatu ya mafunzo ya kiufundi ambayo mada yake ilikuwa 'Kumaliza maafa na zebaki; kulinda usalama na afya kwa wachimbaji madini wadogo' ilikuwa imeandaliwa kwa wachimbaji madini wadogo kutoka Kaunti za Kakamega na Vihiga.

Mwakilishi wa wachimbaji madini, Moses Klay, aliwaomba wafadhili wasaidie wachimbaji kwa mikopo maalumu ili kuwawezesha kuendesha shughuli za uchimbaji madini.

Alitoa wito kwa serikali ya kitaifa iharakishe vibali kwa wachimbaji madini, mojawapo la mahitaji katika kupata mikopo.

Mbunge Mteule wa Bunge la Kaunti ya Kakamega Victorine Shikutwa alisema kaunti imeshughulikia suala la ajira ya watoto katika uchimbaji wa dhahabu.

REPUBLIC OF KENYA

KENYA NATIONAL INNOVATION AGENCY

KeNIA — Kenya National Innovation Agency

VACANT POSITIONS ADVERTISEMENT

The Kenya National Innovation Agency (KeNIA) is a State Corporation established under the Science Technology and Innovation (ST&I) Act, No 28 of 2013 with the mandate to develop and manage the National Innovation System.

The Agency invites applications from suitably qualified applicants to fill the following vacant position:

| S/NO | DESIGNATION | GRADE | NO. OF POSTS | ADVERT NO | TERMS OF SERVICE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Manager Internal Audit | KeNIA 3 | 1 | KENIA/1/2024 | Permanent |
| 2. | Principal Legal Officer | KeNIA 4 | 1 | KENIA/2/2024 | Permanent |
| 3. | Senior Innovation Officers | KeNIA 5 | 2 | KENIA/3/2024 | Permanent |
| 4. | Innovation Officers | KeNIA 6 | 3 | KENIA/4/2024 | Permanent |
| 5. | Senior Office Administrator | KeNIA 6 | 1 | KENIA/5/2024 | Permanent |
| 6. | Assistant Records Officer | KeNIA 8 | 1 | KENIA/6/2024 | Permanent |

**HOW TO APPLY**

1. The details of the posts and mode of application can be accessed on the KeNIA website, https://kenia.go.ke/careers.
2. Interested and qualified persons are requested to submit their applications through the portal.
3. Applications close on 10th December 2024 at 1700hours. Only shortlisted candidates will be contacted.
4. The Kenya National Innovation Agency is an equal employer.

***People with Disabilities, The Marginalized and The Minorities Are Encouraged to Apply.***

REPUBLIC OF KENYA

GDC Geothermal Development Company — Geothermal, Green Energy for Kenya

PUBLIC NOTICE

ALL GDC SUPPLIERS / PROSPECTIVE SUPPLIERS/ GENERAL PUBLIC

NOTICE OF FRAUD

The above subject matter refers.

It has come to our attention that fraudsters purporting to be GDC employees are defrauding the public through false promises of awarding them tenders and LPOs.

GDC wishes to notify the public that tenders and LPOs are issued through GDC's official communication channels after successfully participating in a tender process. GDC further wishes to encourage members of the public to report such persons that contact them claiming to be from GDC and or confirm the same with our GDC office through telephone no. **+254 719 037 000**, email: **info@gdc.co.ke** and anticorruption portal on GDC website: **www.gdc.co.ke/anticorruption/**.

In case of any clarification, please do not hesitate to contact the undersigned or report to our **Hotline No +254 716 888 343.**

**MANAGING DIRECTOR & CEO**

KENYA VISION 2030

Kawi House, South C Bellevue Popo Lane, Off Red Cross Road P.O BOX 100746-00100, Nairobi

**T:** +254(0)719 036 000
**E:** info@gdc.co.ke

www.gdc.co.ke

# Serikali kuangalia upya aina 42 za ushuru zinazoathiri sekta ya chai nchini

NA **FATMA SAID,** KNA

Serikali itachunguza upya ushuru mwingi unaoathiri sekta ya chai, ikibaini kuwa bidhaa za chai kwa sasa zinatozwa aina 42 tofauti za ushuru 42.

Katibu Mkuu wa Kilimo (Dkt. Paul Ronoh amesema kwamba, ili kurahisisha mzigo na kuongeza ushindani katika sekta hiyo, Wizara ya Kilimo inakusudia kutathmini upya kodi hizo na kulainisha mikakati ya uuzaji wa zao hilo michakato nje. Hii ni pamoja na kuboresha mitambo ya kukagua inayotumiwa katika usafirisha chai nje ili kuimarisha utendakazi na kupunguza gharama.

Akizungumza katika hoteli moja mjini Mombasa wakati wa hafla ya kuadhimisha miaka 100 ya uuzaji chai ya Bodi ya Chai Kenya, Ronoh alisisitiza kuwa serikali iko imejitolea kuimarisha sekta ya chai chini ya mpango wake wa ajenda BETA. Mpango huo ni pamoja na mbolea ya ruzuku, maabara mpya ya ubora wa chai, na mkakati wa kutafuta masoko ya kimataifa ili kuzidisha mauzo ya nje ya chai ya Kenya.

Hafla hiyo ilileta pamoja wajumbe kutoka nchi kuu zinazozalisha, kuagiza na kuuza nje chai, pamoja na wahusika wakuu wa sekta ya chai duniani.

Pia ilitoa fursa ya kuwezesha kubadilishana itikadi na taarifa za hivi punde kuhusu chai kimataifa na mustakabali wake.

"Tunapoendelea na kongamano hili la siku tatu za sherehe, tutaweka mikakati ya jinsi tunavyoweza kushughulikia vyema zao hili kwa miaka mingine 100 mingine, na mtazamo wetu na mada yetu ni 'kumfanya mkulima mfalme," akasema.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Dkt. Paul Ronoh (Kulia) alipozuru vibanda vya maonyesho wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 100 ya Bodi ya Chai ya Kenya (TBK) jijini Mombasa. Picha na Andrew Hinga.

Katibu alisisitiza umuhimu wa kuongeza mapato ya wakulima kwa kufanya chai kuwa na faida, akibainisha kuwa tathmini ya kodi ni muhimu kwa sababu inaambatana na mipango ya serikali ya sasa.

"Katika mjadala wetu, tumeangalia wakulima 834,000 ambao ni wachangiaji wakubwa katika sekta hii na ambao pia wanaathiri familia karibu 6.5 milioni. Kwa kuzingatia takwimu hizo, ni wazi kwamba hili ni zao muhimu la kuleta mabadiliko katika uchumi wetu na maisha ya Wakenya, " akaongeza.

Alisisitiza hamu ya kuzingatia zaidi kilimo cha chau ili iwe zao muhimu kwa mabadiliko yetu ya kiuchumi.

Ronoh aliongeza kuwa mbinu nyingine muhimu ni kuongeza thamani, inayozingatia kuuza nje chai iliyosafishwa zaidi badala ya wingi.

Alisema serikali inajenga viwanda vya kutayarisha zao hilo vitakachotumiwa kwa pamoja na wakulima, na kwamba ujenzi huo unaendelea katika kwa sasa maeneo matatu.

Katibu Mkuu alisema viwanda hivyo vitawezesha utayarishaji na upakiaji, kuhakikisha kwamba chai haitauzwa kwa jumla, hali ambayo imesababisha thamani duni katika siku za awali.

Alisema uuzaji wa chai iliyotayarishwa unalenga kuongeza kwa kiasi kikubwa faida na kuvutia masoko ya kimataifa.

Aliongeza kuwa utafutaji wa masoko pia ni mbinu nzuri akibainisha kuwa ili kupanua soko, wauzaji wanahitaji kukumbatia mpango wa mauzo ya kimkakati ya chai badala ya kutegemea minada ya jumla pekee.

REPUBLIC OF KENYA

**The Kiambu National Polytechnic**
**P.O Box 414-00900 Kiambu**
**Tel 020 3522550, 0727807713, 0734207663**

**JOB VACANCIES ADVERTISEMENT**

The Governing Council, Kiambu National Polytechnic (KINAP) wishes to recruit officers in the following areas;

| S/No. | Advert No. | Position | No. of Posts |
|---|---|---|---|
| 1 | Advert No. KINAP/HR/14/2024 | Deputy Supply Chain Officer | 1 |
| 2 | Advert No. KINAP /HR/15/2024 | Counsellor | 1 |
| 3 | Advert No. KINAP/HR/16/2024 | Accountant | 1 |
| 4 | Advert No. KINAP/HR/17/2024 | Driving Instructor | 1 |
| 5 | Advert No. KINAP/HR/18/2024 | Secretary | 2 |
| 6 | Advert No. KINAP/HR/19/2024 | Customer Care Officer | 1 |
| 7 | Advert No. KINAP/HR/20/2024 | Technicians ICT | 2 |
| 8 | Advert No. KINAP/HR/21/2024 | Technician-Fashion and Cosmetology | 1 |
| 9 | Advert No. KINAP/HR/22/2024 | Electrician (Re-advertisement) | 1 |
| 10 | Advert No. KINAP/ HR/23/2024 | Carpenter (Re-advertisement) | 1 |

For detailed Job Description and Job Specification (requirements) log in to our website: **www.kiambupoly.ac.ke**
Application process: **send your current CV, Academic and Professional Certificates including KCSE and Testimonials to: Chief Principal, Po. Box 414-00900, Kiambu, on or before C.O.B Friday 6th December, 2024 in a brown, A4 envelope clearly sealed and with the advert reference number clearly indicated.**

**DELIVERY MODE:** Hand delivery, Post Office or Courier. All applications MUST be received at the Chief Principals office and recorded in the provided book.

We shall not be responsible for loss of hand delivered documents not registered in the provided book.
Only shortlisted candidates will be contacted.

***KINAP is an equal opportunity employer; women, youth and people with disabilities are encouraged to apply.***

**The Chief Principal**
**Kiambu National Polytechnic**
**P.O. Box 414–00900,**

ISO 9001:2015 Certified
TVETA Accredited
Offering Skills for Self Reliance since 1973

KEBS Kenya Bureau of Standards
Standards for Quality life

Tel: 0206948000 | Toll Free Line 1545 | E-mail: info@kebs.org | www.kebs.org

**NOTICE ON FRAUDULENT ACTIVITIES BY KEBS IMPERSONATORS**

It has come to our attention that entities going by the name ***MQA Certification Kenya Ltd*** and ***MQA Certification UK Ltd*** are purporting to have been approved by the Kenya Bureau of Standards (KEBS) to issue the certifications in Kenya.

Kindly note that KEBS has not issued any such approval and neither is it in any way affiliated with these entities. The false statements therefore must be read as a manifest intention to defraud the public. The public is notified and cautioned against engaging with the said entities with respect to any certification services provided by KEBS.

Any person seeking certification in Kenya is invited to visit the KEBS website; **www.kebs.org** or KEBS offices across the country for necessary information.

MANAGING DIRECTOR

#WajibikaNaKEBS
Verify the authenticity of KEBS quality marks by use of the KEBS Official Mobile App or sending a text to 20023: SM#Permit Number / ISM#UCR Number / DM#Permit Number

**KEBS implements an Anti-bribery Management Policy accessible through KEBS Website www.kebs.org**

www.kebs.org
KENYA VISION 2030

# Owalo azuru Mombasa na Lamu kukagua miradi ya inayoendelea

NA **MOHAMED HASSAN,** KNA

Naibu Mkuu wa Itifaki, Usimamizi wa Utendakaji na Utekelezaji katika Ofisi Kuu ya Rais, Eliud Owalo, ameanza ziara ya kukagua miradi ya miundomsingi inayoendelea katika kaunti za pwani za Mombasa na Lamu.

Owalo aliambia wanahabari kwamba lengo la ziara hiyo ya maendeleo ni kukusanya taarifa za moja kwa moja, kutathmini maendeleo ya kazi za ujenzi kufikia sasa, na kutathmini hali ya miradi iliyopo.



**Naibu Mkuu wa Itifaki katika Ofisi Kuu ya Rais, Usimamizi wa Utendaji na Utekelezaji Eliud Owalo akihutubia wanahabari jijini Mombasa.**

Owalo alifichua kwamba ziara pia itatoa fursa ya kuingilia kati kutatua changamoto zinazokabili wanakandarasi na jamii zilizoathiriwa na miradi hiyo.

"Tuko hapa katika eneo la pwani kukagua miradi mbalimbali ya ujenzi inayotekelezwa na serikali ya kitaifa katika kaunti za Mombasa na Lamu," akasema na kuongeza kwamba serikali imechukua hatua za kupunguza hali ngumu ya kiuchumi nchini na itaendelea kutoa miundomsingi muhimu kwa wananchi.

Owalo aliandamana na Katibu Mkuu wa Jinsia na Ushirikiano, Anne Wang'ombe, Kamishna wa Mkoa wa Pwani, Rhoda Onyancha, Kamishna wa Kaunti ya Mombasa, Mohamed Noor, na Sherry Ariko, anayesimamia Utekelezaji wa Huduma za Serikali (GDS) katika eneo la pwani.

Owalo alisema ukaguzi wa eneo la mradi ni muhimu kutokana na mamlaka ya afisi yake ambayo inasimamia kazi ya usimamizi wa utekelezaji wa serikali ya kitaifa.

"Serikali imejitolea kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya miundomsingi ya hali ya juu," akasema.

REPUBLIC OF KENYA

Kenya Power

## INVITATION TO TENDER

Kenya Power invites tenders from interested bidders for provision of the following:-

| TENDER NO. | ITEM DESCRIPTION | TENDER COMMENCEMENT DATE | TENDER CLOSING DATE |
|---|---|---|---|
| KP5/9A/3/10/OT 02/24-25 | Fleet Repair & Maintenance Services from Third Party Garages for Mt. Kenya Region | Wednesday 20.11.2024 | Wednesday 11.12.2024 at 10.00 a.m. |

Tender documents detailing the requirements of the above tender may be obtained from the Kenya Power website (**www.kplc.co.ke**) from **the date shown above.**

**GENERAL MANAGER**
**SUPPLY CHAIN & LOGISTICS**

**www.kplc.co.ke**

DIAL *977# | Access Kenya Power services fast and easy

www.kplc.co.ke | Customercare.kplc.co.ke | Kenya Power | @KenyaPower | 97771 | 0703-070 707, 0732-170 170

OPEN UNIVERSITY OF KENYA

## OFFICE OF THE DEPUTY VICE CHANCELLOR (ACADEMIC AFFAIRS)

**P. O. Box 2440-00606 NAIROBI**
**Email: info@ouk.ac.ke**
**Tel: 020 2000211/2**

## ANNOUNCEMENT OF THE 1ST GRADUATION CEREMONY

## FRIDAY, 29TH NOVEMBER, 2024

The Open University of Kenya (OUK) wishes to inform ALL students who qualified for the award of Postgraduate Diplomas in the 2023/2024 Academic Year, that the 1st Graduation Ceremony will be held on Friday, 29th November, 2024 commencing at 9.00am at the Konza Technopolis Grounds in Machakos / Makueni Counties.

1. **GRADUATION REGISTRATION**

   All graduands are expected to register for the Graduation with their respective Schools after confirming that they have met all requirements including payment of fees. They are also required to confirm the accuracy and order of their names by **Thursday, 21st November, 2024.**

2. **CONVOCATION FEES AND GRADUATION ATTIRE**

   Graduands are required to pay convocation, alumni registration and hire of graduation attire fees. The attires will be available for collection from their respective Schools starting from Monday, 25th November, 2024. The fees are as follows:

| Category | Convocation Fee (Kshs) | Alumni Registration Fee (Kshs) | Graduation Attire Fee (Kshs) | Total (Ksh) |
|---|---|---|---|---|
| Postgraduate Diploma | 2,500.00 | 1,000.00 | 1,500.00 | 5,000.00 |

**Note:** Graduands are required to return the graduation attires by Monday, 9th December, 2024 thereafter a daily fee of Kshs 1,000 will be charged, including weekends and public holidays.

3. **PAYMENT PROCEDURE**

   All payments should be made through e-Citizen system via the student's portal **https://my.ouk.ac.ke**

4. **INVITATION CARDS**

   Graduands will be provided with electronic invitation cards for their guests. University invited guests will also be provided with electronic invitation cards.

5. **PUNCTUALITY**

   Graduands and guests are requested to be seated by 8:30 a.m. on the Graduation Day.

6. **REHEARSAL**

   Graduands are expected to attend the rehearsal on **Thursday, 28th November, 2024 commencing at 10:00 a.m.** in full graduation attire at the Konza Technopolis Grounds.

**For further information, please contact:**
**Office of the Registrar (Academic Affairs)**
**Telephone: 020-2000 211 / 020-2000 212**
Email: **info@ouk.ac.ke**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

GDC Geothermal Development Company — Geothermal, Green Energy for Kenya

## TENDER NOTICE

The Geothermal Development Company Limited (GDC) invites sealed tenders from eligible candidates for the following:

| TENDER NO. | TENDER DESCRIPTION | TARGET GROUP | TENDER SECURITY AMOUNT | CLOSING DATE |
|---|---|---|---|---|
| GDC/INFRA/OT/021/2024:2025 | Tender for Supply and Delivery of Welding Generator | Open to All | Ksh 200,000.00 | 09.12.2024 at 11.00am |
| GDC/INFRA/OT/022/2024:2025 | Tender for Supply and Delivery of High lift Multi Stage Centrifugal Pump | Open to All | Ksh 100,000.00 | 10.12.2024 at 11.00am |
| GDC/EM/OT/023/2024:2025 | Tender for Provision of Service and Supply of Breakdown Parts for Sullair Compressor, Booster & Swivel | Open to All | Ksh 300,000.00 | 11.12.2024 at 11.00am |
| GDC/SC/OT/024/2024:2025 | Tender for Provision of Air Ticketing Services for a Period of two (2) Years Through Framework Contract | AGPO | Tender Securing Declaration Form | 13.12.2024 at 11.00am |
| GDC/EM/OT/027/2024:2025 | Tender for Supply and delivery of ZJ70D Rig Breakdown Parts | Open to All | Ksh 200,000.00 | 16.12.2024 at 11.00am |
| GDC/GRM/OT/030/2024-2025 | Tender for Supply and Delivery of Valves, Equipment and Accessories for Menengai Steam Gathering System | Open to All | Ksh 500,000.00 | 17.12.2024 at 11.00am |

Interested eligible bidders may obtain further information and inspect the tender document from the office of Manager, Supply Chain at Kawi House, South C off Mombasa Road, Red Cross Road between 9.00am and 4.00pm during week days. A complete set of the tender documents may be obtained by interested firms upon payment of a non-refundable fee of Kshs.1000 payable to our accounts office in cash or by banker's cheque. The documents can also be viewed and downloaded from the website **www.gdc.co.ke** or PPIP Portal **www.tenders.go.ke** ***free of charge***. Bidders who download the tender document from the website **MUST** forward their particulars immediately to **procurement@gdc.co.ke** for records and any further tender clarifications and addenda.

The completed tenders in plain sealed envelopes clearly marked with **Tender No.** and **Tender reference name;** shall be addressed to:

**Managing Director & CEO,**
**Geothermal Development Company**
**P.O Box 100746-00101**
**NAIROBI, KENYA**

and deposited in the tender box at Ground Floor GDC office Kawi House, South C Off Mombasa Road, Red Cross Road on or before the dates specified above.

Tenders will be opened immediately thereafter in the presence of the tenderers or their representatives who choose to attend at Kawi House, South C GDC Board Room Ground Floor.

Late tenders will not be accepted.

**MANAGER, SUPPLY CHAIN MANAGEMENT**

KENYA VISION 2030

Kawi House, South C Bellevue Popo Lane, Off Red Cross Road P.O BOX 100746-00100, Nairobi

**T:** +254(0)719 036 000
**E:** info@gdc.co.ke

**www.gdc.co.ke**

# PPB yaapa kukabiliana na biashara haramu ya dawa

NA **ANNE MWALE AND MEGG NJOKI,** KNA

Bodi ya Dawa na Sumu (PPB), kwa ushirikiano na Huduma ya Kitaifa ya Polisi (NPS), imeanzisha operesheni ya kuondoa usambazaji, uuzaji wa jumla na usafirishaji wa dawa ambao haujaidhinishwa katika juhudi mpya za kuimarisha udhibiti wa dawa kote nchini Kenya.

Bodi imeelezea wasiwasi wasiwasi wake kuhusu usafirishaji wa dawa kwa magari maalumu ya usafirishaji, pikipiki na hata magari ya usafiri wa umma bidha leseni na idhini inayohitajika.

Mkuu wa Usambazaji Bora katika PPB, Julius Kaluai, amesema bodi hiyo inashirikiana na Huduma ya Kitaifa ya Polisi (NPS) kuhakikisha kwamba wauzaji wa jumla, wasambazaji na wasafirishaji wasio na leseni ni lazima watimize masharti na viwango vya kitaifa vilivyowekwa la sivyo wachukuliwe hatua za kinidhamu.

“Uamuzi wetu wa kushirikiana na wakuu wa polisi kutoka kaunti zote 47 unafuatia ukaguzi wa hivi majuzi nchini kote wa vituo vya afya uliolenga kubaini na kushughulikia makosa katika sekta ya dawa,” akasema.

Akizungumza mjini Nakuru, Kaluai aliongeza kuwa data iliyokusanywa wakati wa ufuatiliaji itasaidia kutambua mwelekeo katika shughuli za dawa haramu, na hivyo kuwezesha utekelezaji wa kijasusi kukabiliana kikamilifu na masuala hayo.

Pia alisisitiza haja ya ushirikiano wa karibu kati ya PPB na mashirika mengine ya serikali katika maeneo ya mpaka ili kuzuia kuingia kwa dawa ambazo hayajasajiliwa, kuimarisha zaidi ulinzi kwa afya ya umma.

Kaluai alitahadharisha maduka ya reja reja yanayoendesha biashara ya dawa ya mtandaoni ambayo haijaidhinishwa akiwataka wenyewe wasajili majengo yao kulingana na huduma wanazotoa.

Alionya kuwa maduka yote yasiyofuata sheria yatakabiliwa na hatua kali za utekelezaji ili kulinda uadilifu katika usambazaji wa dawa.

Alidokeza kuwa Bodi imependekeza sheria na kanuni kadhaa zitakazosimamia huduma za maduka ya dawa mtandaoni.

Kaluai alisema sheria za awali hazizingatii huduma za afya zinazotolewa mtandaoni na kwamba wanataka kuinua viwango vya sheria zao ili kuwiana na viwango vya kimataifa.

Alisema kuwa maduka ya dawa ya mtandaoni yanakua kwa kasi sana, na kwamba watu wengi wameanza kutumia huduma za mtandaoni.

Aliongeza kwamba ushauri, uuzaji wa dawa, maagizo, na usimamizi wa tiba ni miongoni mwa huduma zinazotolewa kwa njia ya mtandao na wataalamu.

Kaluai alieleza kuwa kuna dawa zinazofaa kuuzwa moja kwa moja katika maduka na nyingine ambazo zinatokana na maagizo ya madaktari pekee. Dawa za maagizo ya madaktari zina sheria kali zinazolinda matumizi yake ili zisitumike vibaya.

